



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
BARAZA LA UUGUZI NA UKUNGA TANZANIA



TAARIFA KWA UMMA

Yah: **UTOAJI WA VYETI VYA USAJILI NA LESENI BAADA YA
MAHAFALI YA NANE (8) YATAKAYOFANYIKA
TAREHE 28 JULAI, 2023.**

Baraza la Uuguzi na Ukunga ni mamlaka ya Kisheria iliyoanzishwa kwa ajili ya kusimamia Wataaluma na Taaluma za Uuguzi na Ukunga ili kuulinda umma dhidi ya huduma zinazotolewa na Wauguzi na Wakunga nchini. Baraza linafanya kazi chini ya Sheria ya Uuguzi na Ukunga ya mwaka 2010 na Kanuni zake.

Ofisi ya Msajili inapenda kuwataarifu Wauguzi na Wakunga waliofanya mtihani wa Usajili na Leseni tarehe 25 Mei, 2023 na kufaulu ila hawatoweza kuhudhuria kwenye mahafali ya 8 ya Kitaaluma kwa sababu zilizo nje ya uwezo wao watatakiwa kufika Ofisi ya Msajili, **Jengo la Kambarage, Barabara ya Mkapa, Ghorofa ya 5, kuanzia tarehe 14 Agosti, 2023** kuchukua vyeti hivyo na vitaendela kutolewa siku na masaa ya kazi (Jumatatu hadi Ijumaa, saa 02:00 Asubuhi hadi 10:00 Jioni).

Aidha, wahitimu wote watatakiwa kuja na Kitambulisho cha NIDA, mpiga kura au Leseni ya Uuguzi na Ukunga ambavyo vitatumika kama utambulisho wakati wa kuchukua vyeti na leseni ambavyo **vitatolewa kwa muhitimu mwenyewe tu, hairuhusiwi kuchukuliana.**

Kwa taarifa Zaidi tafadhali piga simu na:-

0682896529, 0758589706, 0628583390,

Nawatakia utekelezaji mwema.

Imetolewa na:
Amama
Agnes Mtawa
MSAJILI